Energy and Water Utilities Regulatory Authority

MAOMBI YA KUREKEBISHA BEI ZA UMEME SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

Utangulizi

1. Mnamo tarehe 24 Februari 2016, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea ombi la kurekebisha bei Na. TR-E-16-005 kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), likiomba kuidhinishwa:

(a) marekebisho ya bei ya umeme kwa kiwango cha asilimia 1.1 kutoka bei ya wastani ya Sh. 274/Uniti hadi Sh. 272/Uniti kaanzia tarehe 1 Aprili mwaka 2016;

(b) punguzo la asilimia 7.9 kutoka bei ya wastani ya Sh. 272.00/Uniti hadi Sh. 250.62/Uniti kaanzia tarehe 1 Januari mwaka 2017;

(c) kujumuisha Tozo ya Fomu ya Maombi ya shilingi 5,000/= katika Mahitaji ya Mapato;

(d) kuondolewa kwa Tozo ya huduma ya kila mwezi ya shilingi 5,520 kwa wateja wa kundi la T1;

(e) kuwa na mabadiliko ya bei kwa mwaka 2016 na 2017 kulingana na mabadiliko ya bei za mafuta, thamani ya fedha, na mwenendo wa mfumuko wa bei.

2. Tarehe 16 Machi 2016 TANESCO waliwasilisha mabadiliko katika maombi yao ya awali kwa kurekebisha bei ya rejea (*reference price*).

3. Katika kuchambua maombi ya TANESCO, Mamlaka ilizingatia Sera ya Nishati; Sheria ya EWURA, Sura 414; Sheria ya Umeme ya mwaka 2008, Sura 131; na Mwongozo wa Uwasilishaji wa Maombi ya Kurekebisha

bei wa EWURA wa mwaka 2009.

Uhalali wa Marekebisho ya Bei

4. Kwa mujibu wa TANESCO, kupitishwa kwa maombi haya kutaliwezesha Shirika kupata fedha za kulipia gharama za uendeshaji na pia kupata fedha za uwekezaji kwenye miundombinu (*Capital Investment Programme - CIP*) na kulifanya Shirika liweze kutekeleza Sera ya Serikali ya kuhakikisha huduma ya umeme inawafikia asilimia 75 ya wananchi ifikapo 2025.

Ushirikishwaji wa Wadau wa Huduma za Umeme

5. Kulingana na Kifungu Na. 19(2)(b) cha Sheria ya EWURA, Mamlaka ilitoa mwito kwa wadau kuwasilisha maoni juu ya uhalali wa maombi ya TANESCO ya kurekebisha bei kupitia vyombo mbalimbali vya habari yakiwemo magazeti na katika tovuti ya EWURA. Uwasilishaji wa maoni (Taftishi) ulianza tarehe 26 Februari, 2016 na kumalizika tarehe 11 Machi, 2016. Mkutano wa kukusanya maoni ulifanyika tarehe 11 Machi 2016 katika ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam.

6. Katika kipindi cha uwasilishaji wa maoni, Mamlaka ilipokea maoni kutoka Baraza la Ushauri la Serikali (GCC), Baraza la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) na wananchi kwa ujumla kuhusu uhalali wa maombi ya TANESCO.

7. GCC imetoa maoni kwamba TANESCO inahitaji kuwa na mipango ya muda mrefu ya kuondoa mitambo ya umeme wa dharura na mitambo inayotumia mafuta ya diseli ambayo imeligharimu shirika pesa nyingi. Pia GCC inaona kwamba, TANESCO isitegemee ruzuku toka Serikalini ili kugharamia shughuli za uendeshaji na badala yake, iwe na mipango mikakati ya kuinua ufanisi wake katika kujitegemea kifedha. Kutokana na ripoti ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inayoishia Disemba 2013, na kwa kuzingatia hali ya kifedha ya Shirika GCC haina uhakika kama TANESCO ilitathmini maombi yake ipasavyo. GCC inafikiria kwamba kama punguzo la bei ya umeme litakubaliwa, hali ya kifedha ya shirika itadorora na kupelekea kushindwa kutoa huduma kwa wateja wake.

8. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) lilipinga

wazo la TANESCO kupata mkopo kutoka Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kulipia madeni yake ambayo ni Sh. 699.5 bilioni kwa sababu hatimaye walipaji wa gharama zinazohusiana na mkopo ni wateja. Baraza lilishauri TANESCO kuomba mkopo kwa ajili ya uwekezaji badala ya uendeshaji na matengenezo, na wakati huo huo ikiongeza juhudi katika kukusanya madeni yake kwa wateja ambayo yanafikia Sh. 374.92 bilioni. Pia Baraza lilipendekeza njia kadhaa za kuongeza mapato na kupunguza gharama za uendeshaji.

9. Kampuni ya Songas haikuafiki punguzo la bei ya umeme kwa sababu hiyo sio njia ya kukabiliana na matatizo ya fedha katika sekta ndogo ya umeme. Badala yake, Songas imependekeza ongezeko la asilimia 19.28 kwa mwaka 2016 na 9.99 kwa mwaka 2017.

10. Kwenye mkutano ulioitishwa na EWURA, wateja wa huduma za TANESCO walikuwa na maoni kuwa punguzo la bei ya umeme linawezekana kwa kufanyika kwa kipindi kirefu, si vyema kutekelezwa kwa muda mfupi kama ilivyopendekezwa na TANESCO. Wananchi wanaona kuwa punguzo hilo la asilimia 1.1, TANESCO haitaweza kumudu gharama zake za uendeshaji. Pia walipendekeza EWURA ijumuishe malimbikizo ya madeni ya TANESCO katika ukokotoaji wa bei.

11. Ndani ya kipindi cha kutoa maoni, TANESCO ilipewa nafasi kuyatolea maelezo maoni ya wadau wa huduma zake na ilijibu kama ifuatavyo: (a) Maombi ya kurekebisha bei yamezingatia mahitaji ya mapato kwa TANESCO yatakayowezesha Shirika kujiendesha kwa kipindi husika (2016/2017); (b) Uamuzi wa kuondoa gharama za huduma umelenga kuongeza uwezo wa mteja katika kununua umeme na pia kuongeza mapato na matumizi ya umeme; (c) Gharama kubwa za uendeshaji za TANESCO zimetokana na utumiaji mafuta katika uzalishaji umeme na umeme wa kununua kutoka makampuni binafsi ya kuzalisha umeme; (d) Ombi la kurekebisha bei ya umeme limezingatia kwamba hali ya mvua itakuwa nzuri na gesi asilia itakuwepo ya kutosha; na (e) TANESCO imeondoa katika biashara mitambo ya umeme wa dharura.

12. Mnamo tarehe 23 Machi 2016, EWURA iliitisha mkutano wa mwisho wa wadau muhimu ikiwa ni pamoja na Wizara ya Nishati na Madini(MEM), Wizara ya Fedha, Wakala wa Nishati Vijijini, Tume ya Ushindani (*Fair Competition Commission*), Baraza la Biashara, Viwanda na Kilimo la Tanzania (*Tanzania Chamber of Commerce Industry and Agriculture*), EWURA CCC, GCC, TANESCO, TPDC, Songas, IPTL na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO). EWURA iliwasilisha muonekano wa bei na namna zilivyokokotolewa na maoni yaliyotolewa yamezingatiwa katika kutoa maamuzi ya mwisho.

13. Mpaka mwisho wa kipindi cha ukusanyaji wa maoni tarehe 11 Machi 2016, Mamlaka imeridhika na maoni yaliyowasilishwa kuwa yataiwezesha kutowa maamuzi ya kina ya ombi la TANESCO.

Uchambuzi na Marekebisho ya bei.

14. Baada ya uchambuzi wa kina, Mamlaka imejiridhisha kuwa ombi la TANESCO la kurekebisha bei kwa mwaka 2016 ni sahihi isipokuwa vipengele vichache vilivyotajwa kwenye Aya ya 15 na 17 ambapo marekebisho madogo yamefanywa ili kuwezesha maamuzi kufanyika. Pia maombi ya mwaka 2017 yameonekana kuwa na mapungufu kama ilivyoelezwa kwenye aya ya 19.

15. Katika kukokotoa mapato yatakayohitajika, EWURA ilitumia utaratibu wa kawaida wa ukokotoaji wa mahitaji ya fedha katika kupata bei ya umeme iliyoidhinishwa. Hali kadhalika, EWURA ilirekebisha mpango wa uzalishaji uliowasilishwa na TANESCO ili uendane na matarajio ya mwaka 2016 kuwa wa mvua nyingi na makadirio ya uniti za umeme zitakazouzwa.

16. Katika uzalishaji kwa kutumia mitambo yake, gharama ya mafuta ilikadiriwa kwa kutegemea matumizi ya nishati (*specific heat rate*) ya mitambo ya TANESCO ikilinganishwa na ufanisi katika mwaka 2014 na mwaka 2015, wakati gharama ya umeme wa kununua ilikadiriwa kwa kutegemeana na bei zilizoainishwa katika mikataba ya kuuziana umeme (Power Purchase Agreements).

17. EWURA ilitilia maanani kwamba uwekezaji kwenye miundombinu (CIP) upate fedha kiasi cha TZS 351.4 bilioni kutoka katika mapato ya uchakavu wa

miundombinu (*depreciation)* na mapato yatokanayo na faida ya uwekezaji (*return on regulatory asset base)* shilingi 351.4 bilioni iliyokokotolewa kwa kutumia wastani wa gharama ya uwekezaji ya asilimia 11.

18. Kulingana na marekebisho yaliyofanyika, jumla ya mapato yatakayohitajika kwa mwaka 2016 ni Shilingi 1,517,179 milioni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali lifuatalo:

Jedwali: Maombi ya Fedha Yaliyoidhinishwa

Aina ya Gharama	2016 Shilingi (Milioni)
Gharama za Uzalishaji kwa Mitambo ya TANESCO	**353,194**
Gharama ya Mafuta/gesi	*296,534*
Matengenezo	*56,660*
Gharama za Manunuzi ya Umeme	**471,290**
Gharama za Mitambo (Capacity Charge)	*261,248*
Gharama ya Mafuta na Nishati (Energy Charge)	*210,043*
Matengenezo – Miundombinu ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme	68,297
Gharama za Wafanyakazi	256,456
Gharama nyinginezo	108,468
Gharama za Kibenki (*Financing Cost*)	97,103
	1,354,808
Uchakavu wa Miundombinu (*Depreciation*)	123,971
Faida ya Uwekezaji (*Return on Investment*)	227,438
	1,706,217
Toa: Mapato Mengineyo	189,038
JUMLA YA MAPATO YANAYOHITAJIKA	**1,517,179**

19. Katika kupitia maombi ya bei za mwaka 2017, EWURA imebaini kuwa vigezo vilivyotumiwa na TANESCO kukokotoa gharama za kuzalisha umeme havikuwa na mwelekeo sahihi. Pia bei ya gesi asilia ya TPDC iliyotumika ni ya mpito inayosubiri ukokotoaji wa bei kulingana na gharama halisi za mradi zinazotarajiwa kufahamika ndani ya nusu ya pili ya mwaka 2016. Kutokana na sababu hizo, maombi ya mwaka 2017 yameahirishwa na TANESCO inatakiwa kuwasilisha upya

maombi hayo kabla ya tarehe 31 Agosti 2016.

Uamuzi

20. Bodi ya Wakurungenzi wa EWURA iliyokaa tarehe 29 Machi 2016 kufanya uamuzi juu ya maombi ya TANESCO iliamua kama ifuatavyo:-

AGIZO Na. 2016-010

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na. 23(2) na 24(2))

SHIRIKA LA UMEME TANZANIA ("TANESCO") AGIZO LA KUREKEBISHA BEI ZA UMEME, 2016

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) la 2016 la Kurekebisha Bei ya Umeme.

Kuanza kutumika

2. Agizo hili litaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Aprili 2016.

Orodha ya Bei na Tozo

3. Orodha ya Bei ya huduma ya umeme na Tozo mbalimbali za TANESCO zitakazoanza kutumika kuanzia tarehe 1 Aprili 2016 zimeainishwa katika Jedwali Na. 1 na 2 katika Agizo hili. Bei zilizoridhiwa zinaonyesha punguzo la kiwango cha asilimia 1.5 hadi asilimia 2.4 kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na bei ya sasa.

4. Maamuzi ya Marekebisho ya Bei za Umeme kwa mwaka 2017 yameahirishwa mpaka TANESCO itakapowasilisha upya maombi hayo kabla ya tarehe 31 Agusti 2016.

Tozo ya Kuwasilisha Maombi

5. Tozo ya kuwasilisha maombi ya kuunganishiwa umeme ya Shilingi 5,000 imefutwa.

Tozo ya Mwezi kwa Wateja wa T1

6. Tozo ya huduma ya Mwezi ya Shilingi 5,520 kwa wateja wa kundi la T1 imefutwa.

Gharama za mafuta, mfumuko wa bei na ubadilikaji wa thamani ya fedha

7. Kufuatana na kifungu cha Sheria ya Umeme ya mwaka 2008, kifungu cha 23(2) na 23(3) yatakuwepo marekebisho ya bei za umeme kutokana na mabadiliko ya bei za mafuta, thamani ya fedha na mfumuko wa bei. Na marekebisho haya yatafanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 7 ya Urekebishaji wa Bei za Umeme ya 2016.

Gharama za Kukata na Kurejesha Umeme

8. Gharama za Urejeshaji huduma ya umeme ni Sh. 7,000/=.

Tozo ya Kurubuni mita za TANESCO

9. Tozo ya kurubuni Mfumo wa Mita za TANESCO (Metering System)

GN No. 63/2011

kwa wateja wa D1, T1, T2, na T3 itakuwa kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Huduma za Ugavi wa Umeme.

Masharti

10. TANESCO itatekeleza masharti yafuatayo:

(a) uzalishaji wa umeme kwa kuanzia na mitambo yenye gharama nafuu "*least cost merit order dispatch*" na kuwasilisha EWURA kila mwezi taarifa ya hali halisi ya uzalishaji ukilinganishwa na mpango wa uzalishaji uliopitishwa kwenye Agizo hili;

(b) kufikia tarehe 30 Juni 2016, itawasilisha EWURA Mpango wa Uwekezaji (CIP) unaoendana na kiasi cha Shilingi 351.4 bilioni kilichochoruhusiwa kulingana na mapato ya uchakavu wa miundombinu (*depreciation)* na mapato yatokanayo na faida ya uwekezaji (*return on regulatory asset base)*;

(c) kufikia tarehe 31 Agosti 2016, itawasilisha upya maombi ya Marekebisho ya Bei za umeme za 2017;

(d) kuwasilisha kwa Mamlaka kila baada ya miezi mitatu viashiria vya takwimu za ugavi na uhakika wa umeme (*reliability*) katika misongo ya 11 kV, 33 kV, 66 kV, 132 kV, na 220 kV kwa kila mkoa kwa ajili ya uhakiki. Takwimu hizi zitatakiwa kuonyesha jumla ya masaa mteja aliyokosa umeme kwa kila njia ya umeme (*feeder*), kukosekana kwa umeme kulikopangwa (*planned outages*), na ambao haukupangwa (*unplanned outages*), idadi ya matukio ya kukosa umeme katika kila feeder, idadi ya wateja wanaohudumiwa na kila njia ya umeme, idadi ya wateja walioathirika na katizo la umeme katika kila njia ya umeme na uniti za umeme ambazo hazikuwafikia wateja kutokana na makatizo ya huduma (*total unserved energy in kWh*);

(e) katika kipindi cha miezi sita (6), TANESCO iwe imewasilisha EWURA mpango wa utekelezaji wa kuimarisha mfumo wa mita (*metering system*) katika mtandao wa usambazaji umeme kwa lengo la kuweza kupima kwa usahihi nishati ya umeme na kukokotoa kiwango cha upotevu wa umeme kwa ufasaha;

(f) katika kipindi cha miezi sita (6), TANESCO ibuni mikakati ya kupambana na uunganishaji umeme usio halali na ucheleweshaji usio wa lazima katika kutoa huduma, kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja;

(g) kuongeza juhudi za kutoa elimu kwa wateja wake kuhusu Mkataba wa Huduma kwa Wateja na kuhakikisha inashughulikia kero za wateja kwa wakati kama inavyoelekezwa kwenye Mkataba wa Huduma kwa Wateja;

(h) wateja wapya wa majumbani walioko maeneo ya vijijini waunganishwe katika kundi la wateja la D1 kupitia mfumo wa njia moja ya umeme;

(i) kuhamisha wateja walio katika kundi la D1 kwenda T1 endapo manunuzi yao katika kipindi cha miezi mitatu mfululizo yatazidi wastani wa uniti 75 kwa mwezi;

(j) kuwasilisha kwa Mamlaka kila robo mwaka taarifa/ripoti ya ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja wake wanaodaiwa na malipo yaliyofanyika kwa watoa huduma wanaoidai TANESCO;

(k) kuwasilisha maombi ya marekebisho ya bei yatokanayo na mabadiliko ya bei za mafuta, mfumuko wa bei na ubadilikaji wa thamani ya fedha; Ukokotoaji wa

marekebisho hayo utakuwa kama ulivyoainishwa katika Kanuni ya 7 ya Kanuni za Kupanga Bei za Umeme za mwaka 2016 (Electricity (Tariff Setting) Rules, 2016);

(l) itawasilisha kwa Mamlaka taarifa ya fedha zilizopokelewa kama ruzuku au msaada kutoka Serikalini au kutoka kwa Wadau wa Maendeleo kwa ajili ya marekebisho stahiki ya bei ya umeme;

(m) kuendelea kuwasilisha kwa Mamlaka taarifa ya kila robo mwaka kuhusu hali ya kifedha na kiuendeshaji kama inavyotakiwa na Mamlaka; na

(n) ifikako tarehe 31 Mei 2016, kuwasilisha kwa Mamlaka mpango wa utekelezaji wa Masharti yote yaliyoko kwenye Agizo hili.

Kufutwa kwa Agizo

4. Agizo hili linafuta Agizo Na. 013-007 la tarehe 10 Disemba 2013 la Shirika la Umeme Tanzania ("TANESCO") na Marekesho ya Agizo yaliyofuata kuhusu Marekebisho ya Bei za Umeme.

JEDWALI NA. 1: BEI ZA UMEME ZILIZOIDHINISHWA

Kundi la Mteja	Aina ya Bei/ Tozo	Uniti	Bei za Sasa	Bei Zilizopendekezwa 2016	Bei Zilizoidhinishwa 2016	% Mabadiliko
D1	Tozo ya kutoa Huduma	TZS/Mwezi	-	-	-	
	Bei ya Nishati (0 - 75 kWh)	TZS/kWh	100	100	100	0.0%
	Bei ya Nishati (Zaidi ya 75 kWh)	TZS/kWh	350	350	350	0.0%
T1	Tozo ya kutoa Huduma	TZS/Mwezi	5,520	-	-	-100.0%
	Bei ya Nishati	TZS/kWh	298	295	292	-2.0%
	Bei ya Mahitaji ya Juu	TZS/kVA/Mwezi	-	-	-	
T2	Tozo ya kutoa Huduma	TZS/Mwezi	14,233	14,233	14,233	
	Bei ya Nishati	TZS/kWh	200	198	195	-2.3%
	Bei ya Mahitaji ya Juu	TZS/kVA/Mwezi	15,004	15,004	15,004	
T3 - MV	Tozo ya kutoa Huduma	TZS/Mwezi	16,769	16,769	16,769	
	Bei ya Nishati	TZS/kWh	159	157	157	-1.5%
	Bei ya Mahitaji ya Juu	TZS/kVA/Mwezi	13,200	13,200	13,200	
T3 - HV	Tozo ya kutoa Huduma	TZS/Mwezi			-	
	Bei ya Nishati	TZS/kWh	156	154	152	-2.4%
	Bei ya Mahitaji ya Juu	TZS/kVA/Mwezi	16,550	16,550	16,550	

Kielelezo

D1: Wateja wa majumbani ambao wana matumizi madogo ya wastani wa uniti 75 kwa mwezi. Matumizi yatakayozidi uniti 75 yatatozwa bei ya juu ya Shilingi 350 kwa kila uniti moja inayozidi. Kwa kundi hili la wateja, umeme unatolewa katika msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V).

T1: Wateja wenye matumizi ya kawaida hususani wateja wa majumbani, kwenye biashara ndogondogo, viwanda vidogo, taa za barabarani, mabango n.k. Umeme unatolewa katika msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V) na njia tatu (400V).

T2: Wateja wenye matumizi ya kawaida ya umeme kupitia 400V na matumizi kwa mwezi ni zaidi ya uniti 7,500.

T3-MV: Wateja walioounganishwa katika msongo wa kati wa umeme (Medium Voltage).

T3 - HV: Wateja walioounganishwa katika msongo mkubwa wa umeme (High Voltage) ikijumuisha ZECO, Bulyanhulu na Twiga Cement.

JEDWALI NA. 2: GHARAMA ZILIZOIDHINISHWA

Namba 1: Gharama katika Mfumo wa Njia Moja ya Umeme

Njia ya Umeme	Bei ya Kuunganisha iliyopendekezwa (TZS)		Bei ya Kuunganisha iliyoidhinishwa (TZS)	
	Bei kwa Mjini TZS (pasipo VAT)	Bei kwa Vijijini TZS (pasipo VAT)	Bei kwa Mjini TZS (pasipo VAT)	Bei kwa Vijijini TZS (pasipo VAT)
Ndani ya Meta 30	272,000	150,000	272,000	150,000
Ndani ya Meta 70 (nguzo moja)	436,964	286,220	436,964	286,220
Ndani ya Meta 120 (nguzo mbili)	590,398	385,300	590,398	385,300

Namba 2: Gharama katika Mfumo wa Njia Tatu za Umeme kwa Mjini na Vijijini

Njia ya Umeme	Aina ya Mita (Dira)	Bei ya Kuunganisha iliyopendekezwa (TZS)		Bei ya Kuunganisha iliyoidhinishwa (TZS)	
		Bei kwa Mjini TZS (pasipo VAT)	Bei kwa Vijijini TZS (pasipo VAT)	Bei kwa Mjini TZS (pasipo VAT)	Bei kwa Vijijini TZS (pasipo VAT)
Ndani ya Meta 30 (cable 16mm^2)	LUKU	772,893	772,893	772,893	772,893
Ndani ya Meta 30 (cable 16mm^2)	AMR				
Ndani ya Meta 30 (cable 35mm^2)	LUKU				
Ndani ya Meta 30 (cable 35mm^2)	AMR				
Ndani ya Meta 70 (nguzo moja)	LUKU	1,058,801	1,058,801	1,058,801	1,058,801
Ndani ya Meta 70 (nguzo moja)	AMR				
Ndani ya Meta 120 (nguzo mbili)	LUKU	1,389,115	1,389,115	1,389,115	1,389,115
Ndani ya Meta 120 (nguzo mbili)	AMR				

Namba 3: Ada ya Maombi ya Kuunganishiwa Umeme

Kundi la Mteja	Ada ya Sasa TZS	Ada Iliyopendekezwa TZS	Ada Iliyoidhinishwa TZS
Wateja Wote	5,000	--	--

Namba 4: Gharama za kufunga mita zilizo haribika au kurubuniwa na wateja

Kundi la Mteja	Maelezo	Tozo iliyopendekezwa (pasipo VAT)	Tozo iliyoidhinishwa (pasipo VAT)
D1& T1	LUKU (Njia Moja)	60,000	60,000
	LUKU (Njia Tatu)	200,000	200,000
	AMR (Njia Tatu)	300,000	300,000
T2	Mita zinazotumia CT	1,200,000	1,200,000
T3	Mita zinazotumia CT/VT	1,200,000	1,200,000

Namba 5: Gharama za Majaribio ya Mita (*Meter Testing Fees*)

Kundi la Mteja	Tozo iliyopendekezwa (pasipo VAT)	Tozo iliyoidhinishwa (pasipo VAT)
D1	20,000	20,000
T1	20,000	20,000
T2	30,000	30,000
T3	50,000	50,000

Namba 6: Gharama za Uunganishaji Umeme wa Muda Mfupi (*Temporary Power Supply Charges*)

Kundi la Mteja	Maelezo	Tozo iliyopendekezwa (pasipo VAT)	Tozo iliyoidhinishwa (pasipo VAT)
T2	Gharama ya Kuunganishwa	Malipo Halisi na 10%	Malipo Halisi na 10%
T3		Malipo Halisi na 10%	Malipo Halisi na 10%
T2	Malipo ya Amana ya Mita	200,000	200,000
T3		500,000	500,000

Namba 7: Malipo ya Amana ya Umeme (*Energy Deposit for Post-paid Meters*)

Kundi la Mteja	Maelezo	Tozo iliyopendekezwa (pasipo VAT)	Tozo iliyoidhinishwa (pasipo VAT)
D1	Njia Moja	30,000	30,000
T1	Njia Moja	30,000	30,000
T1	Njia Tatu	150,000	150,000
T2	Njia Tatu	200,000	200,000
T3	Njia Tatu	500,000	500,000

Dar es Salaam
..... Machi 2016

Felix Ngamlagosi
Mkurugenzi Mkuu, EWURA